

## Maelezo

Je tunaweza kuielezeaje dhambi? Dhambi ni pale tunapojiweka sisi kuwa ni muhimu kuliko kila kitu, kama iliyyo katika dhambi ambapo 'mimi' ndilo neno kuu. Mungu anakuwa amewekwa pembeni – kama amatajwa! Dhambi ni kumuasi Mungu (kwa kujielewa ama pasipo kujielewa) na mwishowe unajengwa uadui na Mungu. Jambo hili linaweza kuonekana katika namna tatu maalum.

- Kwa matendo – mfano usizi ni tendo la dhambi
- Kwa mitazamo – mfano wivu ni mtazamo ya dhambi
- Kwa hali – mfano kutokuwa na wokovu ni hali ya dhambi

Wanadamu kwa asili wametengana na Mungu aliye mtakatifu na mwenye upendo. Wametengana naye kwa matendo, kwa mtazamo na katika hali ya kiroho. Dhambi kimsingi ni uasi dhidi ya ile haki ya Mungu kuwa Mungu wa maisha yetu. Tunachosema kwa ujumla ni kwamba wanadamu hawapendi ile hali ya wao kutokuwa katikati ya maisha yao, hivyo wanamuasi yule ambaye anapaswa kuwa katikati ya maisha yao – Bwana Yesu.

## Mwanzo wa dhambi – Bibilia inasema nini

Wakristo wanaamini ya kwamba ni katika Bibilia tu tunapoweza kuona kwa ufasaha mwanzo wa dhambi. Ukweli juu ya uwepo wa dhambi duniani si rahisi kuupinga, ingawa watu wengi hujaribu kufanya hivyo, na kujaribu kutoa lawama ya kwamba hali ya mwanadamu inatokana na matatizo ya dunia au Mungu mwenyewe! Wekundu wa dhambi tunausoma kila mahali katika vitabu vyta Bibilia.

Mwanzo **2:17; 3:4-13; 18; 19; 13:13**; Hesabu **32:23**; Zaburi **51:5**; Mithali **14:9**; Isaya **1:5; 6; 14:12-14**; Marko **7:20-23**

*Dhambi ya matendo*

Wagalatia **5:17-21**

*Dhambi ya Mtazamo*

Matayo **5:21; 22, 28, 23:28**; Zaburi **66:18**; Luka **18:11-14**; Yakobo **2:8-9**

*Dhambi ya hali*

Yohana **16:8,9**; Yakobo **4:17**; Warumi **7:1-12**; 1 Wakorintho **15:21-22**; 1 Yohana **1:5, 8; 3:4, 8, 5:17-19**

## Dhambi imeenea ulimwengu mzima

Kwa asili mwanadamu anazaliwa akiwa katika hali ya dhambi, ambayo ndiyo hali ya kila mwanadamu, hata kwa wale waliozaliwa kwa mara ya pili. Tazama Yohana 13:10 – Anapozungumzia juu ya kuoga ana maana yule aliyekwisha kupokea wokovu; na anapozungumzia juu ya kuosha miguu ana maana ile hali ya kila mtu hata muumini kutubu dhambi mara mara.

Mtu anapokuwa 'amezaliwa katika ile hali ya dhambi' haina maana ya kwamba watoto wachanga wametenda dhambi yoyote, ila kuna ile hali ya kutokuepukika ya kwamba watatenda dhambi watakapokuwa wamekua kiumri. Watausukuma kando mkono wa kuume wa Mungu usiwaongoze katika maisha yao.

Dhambi ni ugonjwa sugu wa roho na unapaswqa kutakaswa kikamilifu kama tunakusudia kuepuka hukumu – adhabu ya milele inayotolewa na Mungu mwenye haki.

Utakaso na msamaha unatokea kwa wakati mmoja unaotabulika, pale mtu anapojoitoa kwa Yesu kuwa ni Bwana na Mwokozi, yunapoyatoa maisha yetu na siku zetu zote zijazo kwake – na tunaoolewa kutoka katika adhabu ya dhambi zote zilizopita – na hii ni hali endelevu. Hali yetu ya zamani mara kwa mara itajaribu kujirudia, na sisi tunapaswa kuendelea kuomba msamaha wa dhambi mbalimbali. Kuyatoa maisha yetu kwa Yesu inamaana na inapaswa kuwa ni tendo la toba, tendo la kumgeukia Yesu na kuwa mbali na dhambi. Hili ni tendo linalobadilisha maisha, kwa kawaida katika ubatizo, (wakati mwengine kabla ya ubatizo) na baada ya hapo pale inapohitajika – labda kutwa! Dhambi ni kama mzigo. Kama mtu asiposaidiwa kuutua huo mzigo, mzigo huo utazidi kutulemea kwa kadiri siku ziendapo, na kuathiri maisha yetu ya kimwili, kiakili na kijamii na kiuchumi. Hatimaye kuna hukumu. Miiongoni mwa wanadamu wote waliopata kuishi hapa duniani ndiye hakuwa na dhambi.

Warumi **3:9, 23; 5:12; 7:24-25;** Matendo **17:26;** Waefeso **2:1-3;** Waebrania **4:15;** 1 Yohana **3:5**  
1 Petro **2:22;** Mwanzo **3:8-10; 23-24; 6:7;** Isaiah **48:22;** Yoshua **7:10-12; 25-26**

## Dawa ya dhambi iliandaliwa tangu mwanzo wa nyakati

Katika Agano la Kale damu ya nyama aliyechinjwa kwa sadaka ilifanya 'upatanisho' kwaajili ya yule mtu aliyemtoa yule mnyama, kama mtu yule atatubu (hii ina maana ya kwamba, mtu huyu ataacha dhambi zake) na kuamini uwezo wa ile damu ya sadaka. Kwa wakati uliofaa Mungu mwenyewe alikuja katika namna ya Yesu, 'Mwana wa Mtu', 'Mwana kondoo wa Mungu', na kwa hiari alikuwa mara moja tu kwaajili ya dhambi zote za ulimwengu mzima. Tangu Bwana Yesu alipokufa kwaajili yetu, imani juu ya Yesu na hasa juu ya damu yake aliyoimwaga kwaajili yetu, ndiyo njia pekee ya ya kuepuka nguvu na madhara ya dhambi ('mshahara wa dhambi ni mauti'). Matokeo ya mwisho ya dhambi ni hukumu ya milele ahera (pia tazama mafundisho ya Bwana Yesu juu ya mada hii), na hii inamaana kutengwa na Mungu milele.

Ezekieli **18:4, 20;** Isaya **1:13-18;** Matendo **4:12; 13:38;** Yohana **1:29;** Waebrania **9:26-28;**  
1 Yohana **1:7**

Warumi **5:19; 6:11-12, 23**

Copyright © Sovereign World Trust, PO Box 777, TONBRIDGE, Kent, TN11 0ZS, UK  
[www.sovereignworldtrust.org.uk](http://www.sovereignworldtrust.org.uk)

### Publishing and Translation History

First Published in English by Glory to Glory Publications.

Christian Publications International, PO Box 212, Saffron Walden, CB10 2UU - [www.christian-publications-int.com](http://www.christian-publications-int.com)  
Editor Peter Sammons. Contributors Alex Jacob, David M. Moore, Peter Byron-Davies, Greg Stevenson, Peter Sammons  
ISBN English 978-0-9567831-6-5

This Kiswahili translation for Sovereign World Trust by Revd John Y Madinda with permission  
Swahili Edition Published by Sovereign World Trust ISBN - Kiswahili 978-1-908010-12-4